# MOJAWAPO YA KAZI KUBWA YA KIONGOZI WA KIROHO NI KULETA UELEWA SAHIHI WA KIROHO WA MAMBO MBALIMBALI KWA WALE ANAOWAONGOZA.

**Maandiko: MATH. 22: 23 – 33. MARK. 12: 18 – 27**

1. **UTANGULIZI:**

   **Watu wanaweza kupotea kwa sababu kuu mbili:-**

   a. Kutoyajua maandiko
   b. Kutoujua uweza wa Mungu

Tangu wakati Yesu aliposema maneno haya hadi leo; kinachopoteza watu wengi ndicho hiki.

**"kwa Mfano:**

a. **Kutoelewa kwa usahihi kiroho kwamba hapa duniani sisi ni wapitaji na wasafiri na kwamba hapa duniani hatuna makazi ya kudumu kumepelekea** watu wengi kuwekeza nguvu zao nyingi sana hapa duniani badala ya kuwekeza juu Mbinguni. ***Ebr. 13: 14*** (Hakuna mtu mwenye akili na uelewa kamili anayewekeza nguvu zake nyingi kwenye makazi ya muda**. 1Petro 2: 11-** atawekeza zaidi juu Mbinguni- ***Math. 6: 19 – 21;*** "Uraia wetu halisi baada ya kuokoka ni pamoja na Yesu Kristo Mbinguni (***Filp. 3:20), Ebr. 11:9 – 16.*** Na kwa kuwa hapa duniani kwa sasa sisi ni wageni lazima tuishi kwa kujilinda sana na kujiepusha na anasa na uovu wote wa kidunia ambao lengo lake ni kutuangamiza roho zetu. ***2Pet. 2:20***.

*b.* **Kukosa uelewa sahihi wa Kiroho kwamba kila mtu alikuja bila kitu chochote kabisa hapa duniani wakati anazaliwa** na kwamba ikifika saa ya kuondoka (saa ya kufa maana sote tutakufa) au hata kama Yesu atarudi na tukabadilishwa miili hii kamwe hatuwezi kuondoka na kitu chochote cha dunia hiii!!! ***1Tim.*** **6: 6 – 8, Ayub. 1: 20- 22 na Mhub. 5: 13 - 16.** Eneo hili Yesu alilitolea maelezo yaliyowafanya hata wanafunzi wake washituke**. *Luk. 18: 24 – 30 (18-30)***

**Note: Mtazamo wa Wayahudi ulikuwa kwamba Mtu akiwa na mali (tajiri) basi hii ilikuwa ni ishara ya kwamba mtu huyo ana kibali maalumu cha Mungu; na mtu akiwa maskini waliamini kwamba hiyo ni ishara ya kutokuwa na imani na kwamba mtu huyo hampendezi Mungu!!** ***Mith. 10:15, Yoh. 1: 46***

- Yesu ilibidi afundishe sana katika eneo hili maana Wayahudi walikataa kumpokea /kumkubali Yesu kwa sababu amezaliwa katika hali ya umaskini na anatokea Galilaya – sehemu duni na masikini sana katika Israeli!! ***Luk. 16: 10 – 15, 19 – 31, (Mtah. 4: 12 – 16) Math. 13: 53 – 57.***

- Matajiri mara nyingi wanaishi kama watu wasiomhitaji sana Mungu, na wengi ambao wamezama sana katika kutafuta mali, roho zao zimesongwa. **Luk. 8: 14;** mali siyo dhambi, lakini kusongwa na tamaa ya kutafuta mali ni dhambi kama mtume Paulo anavyoeleza katika - ***1Timoth 6: 6 – 11;*** na baadae ukifa unaziacha zote!!
- **Utajiri siyo usalama wetu na wala mtu hatatosheka na fedha kamwe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu tu.** ***2Kor. 3: 5.***
- Ndiyo sababu kila binadamu anamhitaji binadamu mwingine hata kama ana nguvu kiasi gani. Na kamwe hakuna mtu mmoja anayejiweza kwa kila kitu na anayejua kila kitu. ***Mwz. 2:18, 1Kor. 12: 12 – 27.***

c. **Kukosa uelewa sahihi wa kiroho wa kutosha kwamba kuna maisha ya milele baada ya kufa Mbinguni au Jehanamu kunafanya wateule waishi bila tahadhari/umakini. Mark. 9: 42 - 49.** Ukiwa na uelewa sahihi, utapiga na kupinga dhambi katika maisha yako kwa gharama yoyote ile***. Kol. 3: 5 – 10, Efes. 4: 17 - 25.*** **Maana hakuna mtenda dhambi hata mmoja atakayeingia Mbinguni. Ufun. 21: 27.**

***Note:*** ***<u>Maana ya kila mtu kutiwa chumvi kwa moto ni:-</u>***

i. Kukubali kupitia mateso na dhiki katika maisha haya baada ya kuokoka bila kumkana au kumwaibisha Yesu. ***Yoh. 15:18- 21, Math. 5: 11-12, Matendo. 14: 18 – 20, 5: 40 - 42***

ii. Kwa wale wote watakaomkataa Yesu na kujifurahisha katika dhambi katika Ulimwengu huu ambao moto wa Jehanamu usio zimika utawaunguza maunguzo makuu bila kufa milele. ***Mark. 9: 42 -48, Ufun. 20: 1 – 15.***

Lazima kufanya uchaguzi wa kulia sasa ili ucheke baadae milele na milele au ucheke sasa kwa kitambo kidogo na uje ulie milele na milele. **Maisha matakatifu yanaanzia hapa hapa duniani – Zab. 16: 3, na Yesu atarudi ghafla ili kuchukua Kanisa lisilo na mawaa wala kunyanzi. Ikor. 15: 50 - 54, 1Thes. 4: 13 – 18, Ufun. 14: 13, Mdo. 1: 6 – 11; Efes. 5: 25 - 27; Ebr. 12: 1 – 12, Ebr. 11: 32-40, Ayub. 42: 7 – 9.**

d. **Kukosa uelewa sahihi wa kiroho kwamba Yesu alimshinda shetani na akamnyang'anya funguo zote na mamlaka yote kunapelekea watu wengi kundelea kuishi maisha yaliyojaa HOFU na wasiwasi na kuendelea kumtukuza shetani katika maisha yao. Yoh. 19: 30, Kolos. 2: 13 – 15. Math. 28: 18 – 20, Ufun. 1: 17 – 18, Ufun. 5: 1 – 14, n.k**. Mitume na Manabii walipopata uelewa sahihi kuhusu Yesu, hawakubabaishwa tena na dhiki na majaribu waliyokutana nayo na hiyo ikawa siri yao kub wa ya kusimama imara pasipo kuyumbishwa. Mungu atusaidie sana wateule wa sasa katika eneo hili la kumfahamu sana mwana wa Mungu na Bwana ayatie nuru macho yetu ya rohoni katika jambo hili muhimu ili tusiyumbishwe na kutupwa huko na huko kama watoto wachanga na imani potofu zinazozuka leo**.** **Efe**. **4: 13 - 15.** Tukiujua sawasawa uwezo wa Jina la Yesu Kristo, hatutamwogopa kamwe shetani na majeshi yake. **Mdo. 3:6–8, Mdo. 4: 12, 8: 9 –13, 19: 13 - 16** n.k. Mungu awabariki.

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi.***
***June 2021***